

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

121/2

KISWAHILI 2

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shulen)

Muda: Saa 3

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **tano (5)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Ukurasa wa 1 kati ya 3

©CSCE2022

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. "Udhamini wa kazi za fasihi ni muhimu lakini huweza kumwathiri mtunzi wa fasihi." Tetea kauli hii ukieleza faida tatu na athari mbili za udhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi.
2. Kwa kutumia hoja tano na mifano, tathmini umuhimu wa michezo ya watoto kama utanzu mmojawapo wa sanaa za maonesho.
3. Onesha namna vipengele vya muundo, mtindo, sitiari, tashihisi na taswira vinavyojibainisha katika vitendawili.
4. Soma shairi lifuatalo kisha bainisha vipengele vyake vya kifani:

Maisha ya mwanambuzi, si leo tangu kitambo,
Ha'shiwi mapingamizi, mzingiwa na ulimbo,
Wimawima usingizi, mashaka kukimu tumbo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Maisha ya mwanambuzi, thama tuyambe msimbo,
Ni maisha ya gumbizi, tena yananuka shombo,
Ha'chani na vizuizi, uchao hula makombo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Mashaka ya mwanambuzi, mbele kamba nyuma fimbo,
Hubembe'zwa kwa uluzi, mchunga huimba wimbo,
Hapati nafasi mbuzi, kumraruua kiwambo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Majuto ya mwanambuzi, mwanambuzi kawa pambo,
Alikwepa mchuuzi, kwa mchuuzi wa kambo,
Mtego wa mlangazi, kwake mbiu ya mgambo,
Mbele kamba nyumba fimbo, maisha ya mwanambuzi.

Nimefanya uchunguzi, mbuzi mnyonge wa tumbo,
Mbuzi hana uamuzi, maisha yake ni chambo,
Yapekue mpekuzi, maisha yale ni chambo,
Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu** (3) kutoka sehemu hii. Swali la **tano** (5) ni la lazima.

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Kimbunga	-	Haji Gora
Mapenzi Bora	-	Shabani Robert
Chungu Tamu	-	Theobald A. Mvungi
Fungate ya Uhuru	-	Mohamed S. Khatibu.

RIWAYA

Usiku utakapokwisha	-	Mbunda Msokile
Kufikirik	-	Shabani Robert
Mfadhibili	-	Hussein Tuwa
Vuta N'kuvute	-	Shafi Adam Shafi

TAMTHILIYA

Kwenye Ukingo wa Thim	-	Ebrahim Hussein
Morani	-	Emmanuel Mbogo
Kivuli Kinaishi	-	Said Mohamed
Nguzo Mama	-	Penina Muhando

5. Mtunzi bora ni yule anayebainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii. Kwa kutumia mifano mitatu kwa kila diwani, tetea hoja hii kwa kutumia diwani mbili kati ya ulizosoma.
6. "Ujumbe wa kazi ya msanii huwa ndani ya vipengele vya lugha." Fafanua kauli hiyo kwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani ukiongesha jinsi lugha ya picha ilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani mbili ulizosoma.
7. "Harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.
8. Tathmini umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya mbili ulizosoma. Toa hoja nne kwa kila kitabu ukizingatia hoja mbili kwa kila aina ya matumizi.